BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Nne – Tarehe 20 Mei, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Hotuba ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (Bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) kwa Mwaka 2024/2025.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

168. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Tatizo la uharibifu wa mazingira ni la muda mrefu hasa katika visiwa vyetu vidogo vidogo hapa Zanzibar, na moja ya jukumu la Wizara yako ni kufanya tathmini juu ya uharibifu huo.

Je, tathmini iko vipi juu ya suala zima la uharibifu na utunzaji wa mazingira katika visiwa vyetu vidogo vidogo hapa Zanzibar.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

114. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi na Utawala bora:

Katika kuhakikisha utendaji kazi bora wa watumishi wa Serikali, mfumo wa tathmini ya utendaji kazi (Performance Appraisal) ni muhimu katika kuhakikisha uwajibikaji na ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma. Pamoja na mfumo huu kuonekana kufanya kazi vyema katika mataifa mengi na kuongeza ufanisi, bado utekelezeaji wa mfumo huu katika taasisi za umma hapa Zanzibar unasuasua.

(a) Je, ni mifumo gani ya tathmini ya utendaji kazi inayotumika kwa watumishi wa taasisi za umma hapa Zanzibar.

(b) Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuja na mfumo wa kielektroniki wa utendaji kazi (Performance Appraisal) ili kuongeza ufanisi katika taasisi zetu za umma.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

161. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kiasi gani wafanyabiashara wa Zanzibar wanapata unafuu wa kodi kwa bidhaa wanazozisafirisha kwenda Tanzania Bara.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

34. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba iliamua kutenga pesa na baadae kuwapatia mikopo nafuu makundi ya kina mama asilimia (4%), vijana asilimia (4%) na watu wenye mahitaji maalum asilimia (2%). Na kwa kuwa tokea Awamu ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuingia madarakani ilisitisha fedha hizo kutolewa na Halmashauri na badala yake iliielekeza Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji itoe mikopo hiyo na kuweka utaratibu mzuri wa ugawaji wa fedha hizo.

    Na kwa kuwa kimepita kipindi kirefu tangu kusitishwa kwa mikopo hiyo, Je, Serikali imekusanya kiasi gani kwa kipindi ilichositisha kutoa fedha hizo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

17. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

    Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya kutatua na kutafuta ufumbuzi wa changamoto ya maji safi katika sehemu tofauti nchini, bado kuna maeneo hadi leo hii hayapati maji, ikiwa ni pamoja na maeneo ya Chukwani yaliyo karibu na jengo la Baraza la Wawakilishi, upande wa Msikiti Mwekundu, Sumai, kwa Mahita na upande wa Coconut. Vile vile huduma hiyo inakosekana katika shehia ya Chukwani, Kiembesamaki, Mchina, Michungwani na maeneo mengine.

    (a) Je, kwa uhakika upi Serikali inalitambua tatizo hilo.

    (b) Ni nini chanzo cha changamoto hizo.

    (c) Ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inapatikana katika maeneo yote hayo.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

26. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Uzoefu unaonesha kuwa yanapotokezea majanga ya moto na mafuriko, wanafunzi wengi waliohifadhi vyeti vyao majumbani au sehemu inayokumbwa na majanga hayo, hupoteza vyeti vyao vya uhitimu wa masomo yao, hali inayowapa wakati mgumu hasa tukizingatia vyeti hivyo ni muhimu kwa maendeleo yao.

(a) Je, Wizara yako inalichukuliwa vipi suala hili.

(b) Je, Wizara yako inawasaidia vipi wanafunzi ambao wamepoteza vyeti vyao vya uhitimu wa masomo pale wanapotaka kujiendeleza na elimu ya juu.

64. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uamuzi wake wa kuimaliza Skuli ya Msingi ya Tazari, hasa kufuatia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alipoitembelea na kuzungumza na wananchi wa hapo. Hata hivyo, kuna banda bado halijamalizika kujengwa hadi sasa.

(a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inaikumbuka ahadi hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aliyoitoa mbele ya wananchi wa Tazari.

(b) Je, Wizara yako inawapa ahadi gani ya matumaini juu ya skuli yao, hasa wakati huu ambao wanafunzi wanapata tabu.

## Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

175. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Uchumi wa buluu ni nguzo tegemeo la uchumi wa Zanzibar na tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Nane kwa kuanzisha Wizara maalum ya Uchumi wa Buluu kwa dhamira ya kukuza uchumi wetu.

(a) Je, ufadhili wa wanafunzi na wafanyakazi wangapi wa masomo umepatiwa kwa ajili ya kuja kuongeza kasi ya

uchumi wa buluu kwa sasa.

(b) Tutarajie tafiti ngapi na kwenye maeneo yepi, ambazo zitasaidia kuleta suluhisho mbali mbali katika changamoto za uchumi wa buluu hapa Zanzibar.

(c) Kwa kiasi gani suala la uharibifu wa mazingira na ukataji wa mikoko linaathiri maendeleo ya uchumi wa buluu nchini.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

197. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Katika hali ya kuendelea na ujenzi wa nyumba na majengo mbali mbali, kuna muda nyumba na majengo hayo huwa maboma ambayo huachwa bila ya kuendelezwa au hukaa muda mrefu bila ya kumalizwa ujenzi wake.

Nini ipi kauli ya Serikali juu ya maboma mengi yanayotumiwa na wahalifu kuwa ni maficho ya wahalifu ndani ya eneo la 'Jumbi Site Plan' pamoja na uwepo wa vichaka vikubwa vikubwa visivyosafishwa kwa kipindi kirefu sasa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**20 Mei, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**